

KILIMO CHA NANASI



1. Utangulizi wa kilimo cha nanasi

Nanasi ni mmea wa kudumu wenye majani laini, unaokua kati ya sentimita 10 hadi 130 kwa urefu na upana wa sentimita 130 - 150. Mmea huu una shina moja kuu, aina mbili za mizizi, kuna mizizi ya juu na ya ardhini, majani yanayofunika kabisa shina, na pia huweza kutoa machipukizi (suckers) kutegemea aina.

2. Uchaguzi wa Eneo, Mahitaji ya Eneo, na Maandalizi ya Shamba

- Joto: Halijoto inayofaa: chini ya nyuzi joto 36°C na si chini ya 20°C.
- Mvua: Nanasi huvumilia ukame, lakini mavuno hupungua sana pasipo unyevu wa kutosha: Mvua iliyosambaa vizuri kwa mwaka karibia 600mm ni bora.
- Mwanga za wa Jua: Ubora wa tunda unategemea joto la usiku kuwa baridi na mchana wenye jua la kutosha.
- Udongo: Udongo wenye asidi (pH 4.5 – 5.5) unafaa hii huzuia magonjwa ya udongo. Epuka pH ya juu ya 7.0.
- Udongo unapaswa kuwa na mfereji mzuri wa maji, rutuba ya kutosha, na kiasi kizuri cha mbolea ya asili na potassium (K).

Hatua za Maandalizi ya Shamba

1. Kusafisha na kulima shamba.
2. Kutengeneza matuta au mirundo kwa ajili ya mifereji.
3. Kupima udongo na kurekebisha (mfano kuongeza chokaa kurekebisha pH)

Upandaji na Mpangilio wa Mistari

- Nafasi ya 30 x 60 x 90 cm (30 kati ya mimea, 60 kati ya mistari, 90 kati ya matuta).
- Panda mistari 3 au 4 kwa tuta lakini zingatia usimamizi sahihi na matunda madogo ya katikati.
- Muda bora wa kupanda ni mwanzoni mwa msimu wa mvua

3. Uzalishaji wa Miche ya Nanasi (Propagation)


Nanasi huzalishwa kwa njia ya kupandikiza machipukizi manne yafuatayo:

Aina	Upatikanaji	Ufanano	Muda wa kuvuna	Uwezekano wa magonjwa	Kuchanua bila mpangilio
Taji la juu (Crown)	Mara baada ya kuvuna	Sawa	Miezi 18	Rahisi kushambuliwa	Chini
Slip	Baada ya kuvuna	Sawa	Chini ya miezi 16	Chini	Chini
Chipukizi ya juu (Aerial sucker)	Miezi 3-4 baada ya kuvuna	Tofauti sana	Karibia miezi 14	Chini	Rahisi sana
Chipukizi ya chini (Ground sucker)	Miezi 4 baada ya kuvuna	Tofauti sana	Karibia au sawa na miezi 14	Chini	Rahisi sana

<p>Jinsi ya Kupanda kwa Taji (Crown)</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Vua taji kutoka kwa tunda kwa kuizungusha. ➤ Ondoa tabaka 3–4 za majani ya chini. ➤ Kausha kwa siku 3–4. ➤ Panda moja kwa moja kwenye udongo. 	<p>Kwa Slip na Suckers</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Vunja kwa uangalifu kutoka kwenye shina au kati ya majani ➤ Ondoa majani ya chini ➤ Panda
--	---

<p>4. Usimamizi wa Mazao.</p> <p>Kudhibiti Magugu</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Tumia matandazo na palizi ya mkono <p>Mbolea</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Mbolea za asili kama vile mboji, samadi ➤ Ratiba ya kuweka mbolea kwenye shamba, weka kwa awamu kwa mwezi wa 3 na wa 6 baada ya kupanda. <p>Umwagiliaji</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Drip au mifereji wakati wa kiangazi. 	<p>5. Udhibiti wa Magonjwa na Wadudu</p> <p>Wadudu wa kawaida</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Vidukari (mealy bugs), minyoo (nematodes), siafu <p>Magonjwa ya kawaida</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Heart rot, black rot, fusarium wilt <p>Mbinu za Udhibiti</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Tumia njia asilia kama vile mzunguko wa mazao, usafi ➤ Tumia dawa za mimea kama neem ➤ Integrated Pest Management (IPM)
--	--

<p>6. Kupalizi ya maua na kutengeneza matunda.</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Kuchochea maua huanza miezi 8–10 baada ya kupanda ➤ Kukomaa kwa tunda huanza miezi 5–6 baada ya kuchochea maua 	<p>7. Kuvuna na baada ya kuvuna</p> <p>Dalili za kuvuna:</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Mabadiliko ya rangi ➤ harufu nzuri ➤ ukubwa wa tunda.
---	---



Mwisho, kwa mkulima anataka kupata mavuno bora kwa wakati **apande slip** kwa sababu zinakua haraka, zinakinga ya wastani hazichanui mapema.

Crown au taji huchelewa sana na ni rahisi kuaoza.

Sucker zinakua haraka lakini hazifanani kwa ukubwa na zinaweza kuchanua kabla ya wakati. Hivyo slips ni bora zaidi.